

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA

Simu: +255 27- 2641105

Fax: +255 27- 2641414

Barua pepe: ded@muhezadc.go.tz

Tovuti: <http://www.muhezadc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P 20,

Muheza- Tanga

TANZANIA.

TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA (W) MUHEZA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUCHUKUA TAHADHARI YA UGONJWA WA CORONA AMBAO HUENEZWA KUPITIA MAJIMAJI YANAYOTOKA KATIKA NJIA YA HEWA, MDOMONI NA PUANI AMBAYO MTU MWENYE VIRUSI VYA COVID-19 ANAWEZA KUYATOA WAKATI WA KUPUMUA, KUPIGA CHAFYA, KUGUSA MAJIMAJI (JASHO) AU VITU VILIVYOTUMIWA NA MTU MWENYE UGONJWA WA COVID-19 KAMA VILE KITAMBAA, NGUO, KUSHIKANA MIKONO AU VIFAA VINGINE AMBAVYO VIMEGUSWA NA MTU MWENYE VIRUSI VYA CORONA.

DALILI ZA UGONJWA WA CORONA (COVID 19) NI KAMA IFATAVYO

- a) Homa
- b) Mafua
- c) Kuumwa na kichwa
- d) Mwili kuchoka
- e) Kikohozi
- f) Kubanwa mbavu
- g) Maumivu ya misuli
- h) Vidonda vya koo
- i) Kupumua kwa shida hata kifo

MAMBO YA KUZINGATIA ILI KUJIKINGA NA CORONA.

- a) Kuepuka safari zisizo za lazima kwenda, kwenye maeneo yaliyoathirika.
- b) Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa kwa kitambaa safi.
- c) Kuepuka kugusana na mgonjwa mwenye dalili za magonjwa ya hewa mwenye historia ya kusafiri maeneo au Nchi zilizoathirika.
- d) Kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni(sanitizer au antiseptic soap).
- e) Kuwahi kwenye kituo cha kutolea huduma za afya endapo utakuwa na dalili zilizoainishwa. Pia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza amesitisha vibali vya kufanyia sherehe, matamasha na promotion za biashara ikiwa ni sehemu ya kuzuia mikusanyiko isiyo ya lazima.
- f) Toa taarifa ya uwepo wa mtu mwenye dalili za Ugonjwa huu kwenye kituo cha Afya kilichopo karibu nawe au piga simu **0755415152 au 0755757154**
- g) Msiende katika mikusanyiko ya watu (sherehe, misiba , kumbi za starehe na harusi).
- h) Ongea na mtu walau mkiwa umbali wa mita 1 msisogeleane sana.
- i) Msisalimiane kwa kushikana au kukumbatiana.
- j) Tumia muda wako mwingi kukaa nyumbani kwako wakati wa mlipuko/ pindi mlipuko utakapotokea.

IMETOLEWA NA


NASSIB .B. MMBAGGA.

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA

WILAYA YA MUHEZA.

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA
WILAYA YA MUHEZA**